Azimio la mwisho alilochukua Sarah hakika aliona lingekuwa sahihi sana kwake. Hakutaka kujiuliza mara mbili kuhusu uamuzi wa kurejea nyumbani, kwenda kuyasuluhisha mambo baina yake na Allen. Alihisi uwepo wa nguvu fulani ndani yake, iliyomsukuma kuamini kuwa bado alikuwa na nafasi ya kurejesha moyo wa Allen umpende tena.

Aliamni kuwa Allen alimpenda sana, tena alimpenda sana tangu wakiwa watoto. Na ndiyo maana, penzi lao likaweza kudumu kwa miaka mingi hadi walipoufika utu uzima. Hakujua angeweza vipi kusema na Allen juu ya hilo, lakini aliamini kuwa ingefaa sana kama angetumia vema hiyo nafasi kusema naye. Aliamini, kule nyumbani palikuwepo na wazee pia, ambao wangeweza kusimamia suala hilo hadi kurejesha penzi lao lililokufa kiasi cha mwaka mmoja uliopita.

Akaomba ruhusa kwa waajiri wake, yaani Mr Rafael Mwakisu na mkewe, na wao wakampa baraka zote. Sarah akaahidi kuwahi kurejea, mara tu atakapomaliza shughuli inayompeleka kijijini. Sarah, almaarufu kama 'Jojo', akachukua begi dogo tu la mgongoni lililobeba nguo chache, na kuivaa safari. Palipokucha, tayari alikuwa ameshaketi katika siti ya basi la kuelekea nyumbani kwao.

Hadi nyakati za kupooza kwa miale ya jua, tayari Sarah alikuwa ameshawasili katika ardhi yake ya nyumbani. Uchovu ulimzidi kupita kiasi, imichangiwa na mwili wake uliojazwa nyama nyingi za upendeleo. Kiza kililposimika vema mizizi yake, alikuwa amesimama katika mlango wa nyumba aliyoishi na wakongwe, Babu, Bibi pamoja na wadogo zake wawili Bona na Gabi.

Alibisha hodi na kufunguliwa, akaingia ndani. Uchangamfu wa kila mtu ndani ya nyumba ile haukushabihi kabisa na ule wa Sarah. Watu wote walionekana kupoa, wakionesha matabasamu yasiyo na nishati ya kutosha. Kutokana na uchovu, pamoja na usiku kuingia sana, basi usiku ule ulipita pasina wanafamilia hao kusemeshana lolote kuhusu maisha ya mjini. Wakalala kuupisha usiku upite.

Palipokucha, Sarah akawekwa kikaoni. Familia nzima ilikaa kusema naye. Wakaitwa ndogu waeili wa kuzaliwa tumbo moja na marehemu mama yake. Naam, kwa ujumla, kikao kilihusisha jumla ya watu sita, yaani Babu, Bibi, Bona, Mjomba pamoja na Mama Mdogo na Sarah mwenyewe. Wote walionekana kuwa na 'ajenda' moja yenye kukinzana na Sarah. Hatimaye mada ikawekwa mezani.

Yalizungumzwa mengi sana, lakini kubwa zaidi walijadili kuhusu kuporomoka kwa maadili ya binti yao mkubwa. Wakayaweka bayana yale yote waliyokuwa wakiyasikia kwa watu kuhusu maisha ya Sarah huko mjini. Walionekana kusikitishwa sana na kile walichodai kuwa ni 'uasi' na 'kuwavua' nguo. Tabia chafu za biashara haramu ya kujiuza, kubadili wanaume wa mtaa mmoja, marafiki wapotofu, kupoteza haiba na mengine mengi yakasemwa.

"Na sasa, umeenda mjini kutumia madawa ya 'wazungu'. Umebadilika hadi ngozi, mzungu- sio- mzungu..! mwarabu- sio- mwarabu...! chotara- sio- chotara..! Hukuwa hivyo wewe, ona nyuma ukivyojazika...! Mungu wangu...!".

Mama Mdogo akaanza kumchambua Sarah aliyeamrishwa kusimama mbele zao. Bona pamoja na Mjomba wakatazama pembeni kwa aibu, wakikataza macho yao kutomtazama Sarah kuepusha  kutamanisha nafsi zao kwa mtego wa majaribu. Licha ya kujivika Khanga, na kujisitiri mwili wake, lakini bado Sarah alibaki kuonekana sehemu kubwa ya mwili wake. Babu akasikitika, akinong'ona chini chini kwa lugha ya kabila lao. Bibi akaziba mdomo wake kwa mshangao. Hata aliooketi, bado mjadala haukuishia hapo. Ikafuata mada nyingine iliyokuwa ya moto, ni kuhusu mahusiano yake na Allen.

"Umetutia aibu hapa kijijini. Kila mtu anajua kuwa uliachana na kijana wa Mzee Bingwa kwa kuendekeza umalaya.". Alisema Mama Mdogo.

"Ndiyo, sisi tukijikuta kwenye mgogoro na familia ya Mzee Bingwa. Walidai kurejeshewa mahari aliyolipa kijana wao...! Ulipita muda mrefu sana bila kumaliza hii kesi, hadi serikali ya kitongoji ikaja kuingilia kati". Bibi nae akachangia neno lake.

Lilipogusiwa suala la kumuhusu Allen, basi kila mtu alimshamhia Sarah kwa maneno ya lawama kwa kile walichokiita ni 'kukosa adabu' na kuwafedhehesha wanafamilia wote. Sarah ambaye aliyajua makosa yake, alibaki kimya kuruhusu nduguze wamalize makasiriko na dukuduku zinazowakaba. Alitulia kwa maana pia alifahamu dhahiri kuwa ni yeye ndiye mkosaji, na yasemwayo ni ya kweli kabisa. Kimya chake kilikwenda sambamba na majuto makuu.

Baadaye kidogo, baada ya kupita kwa masaa mengi ya kikao, Sarah alitoka pekee yake na kuelekea mtoni, eneo la mbali kabisa na maeneo ya kijijini kwao. Alipofika huko, akatafuta kivuli tulivu na kuketi. Licha ya kuufaidi upepo mwanana wenye harufu ya majani mabichi yapatikanayo kwa wingi mtoni hapo, licha ya kuyafurahia mandhari kwa upekee, lakini nafsi yake ilitokota bado.

Alizikumbuka zile nyakati za dhahabu, alipokuwa akicheza na Allen katika viunga hivyo. Aliyakumbuka yote kwa usahihi. Ni katika machaka ya mto huo, ndipo alipompa Allen zawadi ya tunda kwa mara ya kwanza, enzi hizo alipokuwa binti kigori. Ni katika siku hiyo, ndipo Allen alipoutoa usichana wa Sarah.

Eneo lile lilimkumbusha mengi sana bibie Sarah, kwa maana lilikuwa eneo lake pendwa na la kipekee kuliko maeneo yote ya kijijini hapo. Kila mara alipoyatazama mandhari, alizikumbuka zile ahadi za kuoana ma kuzaa watoto na Allen. Alijiinamia na kulia sana.

*                    *                    *

Sarah alijiketisha na kusuhiri jambo lake litimie. Alikuwa akisubiri kumuona mmoja

kati ya watu alioamini wangeweza kumpokea yeye pamoja na hali yake kisha kumsitiri. Alikuwa akimsubiri aliyekuwa rafiki yake wa toka zama hizo, Rose. Na kweli, subira yake ikazaa matunda. Baadaye kidogo, Rose alipita tena njiani hapo akitokea kisimani. Sehemu mbalimbali za mavazi yake zilionekana kulowa, kutokana na shehena ya maji iliyohifadhiwa mtungini kutotulia katika ngata.

Sarah alimsimamisha na kumuomba azungumze naye. Na wakasimama njiani kuzungumza kama walivyokubaliana.

"Pole, mwaya. Naona maji yamelowanisha nguo zako..!".

"Asante, nakusikiliza shida yako..!". Aliuliza Rose, akizungumza kwa ufupisho sana na hakuonekana kumfurahia Sarah.

"Mwenzio nimekukumbuka sana, rafiki yangu..! Imekuwa muda mrefu bila kuonana na wewe, jamani..!".

Badala ya kujibu, kwanza Rose alimtazama Sarah kwa jicho kali kuonesha kutokuwa na masihara tena baina yao. Jicho lile lilimtisha Sarah, naye akapwaya kidogo kuona Rose amekuwa 'bandidu' kiasi kile. Akaona atumie ukimya wa Rose kumpa neno lingine.

"Naomba unisamehe tu, mwaya. Nimegundua kosa langu na nimeona wapi nilipoteleza. Sitokuwa na amani kama sitopata msamaha kutoka kwako, shoga yangu..!".

"Leo yamekusibu yapi, hadi unaniita rafiki yako..!? We' si ndiye uliyenitamhia kwenye simu ukinisema kwa ushamba wangu..!? Si ni wewe uliyechamba nilipokuuliza kuhusu Allen..??".

"We' acha tu, Rose. Dunia imenipa funzo kubwa lililonisafisha jicho. Nitatafuta wakati mwingine mzuri zaidi nikusimulie. Kwa sasa naomba upokee msamaha wangu..!".

"Ulimbukeni umekutia aibu, eeenhh..? Sasa nami sina muda wa kuongea na wewe, maana ulishasema kuwa mimi siyo wa kuwekwa sahani moja na wewe..,!!". Rose alijibu kwa ujeuri na maringo. Macho yake yakateleza kwenda juu na kushuka chini, akimtazama Sarah katika namna iliyotangaza dhahiri kuwa hakutishwa na uzuri wake wala chochote alicho nacho.

Sarah alijisikia aibu sana. Hata ujasiri wa kuendelea kuzungumza na Rose ukamuisha na kupotelea asipopajua. Akiwa anajifikiria kutamka lolote, mara Rose akatoweka mbele yake katika namna ambayo pasina shaka haikuwa njema kwa Sarah. Hilo lilikuwa pigo kubwa lingine kwa Sarah. Aliona kila mtu akigeuka na kuwa kinyume naye. Kila mtu alichukizwa na madudu yake, awali walikuwa ndugu zake na sasa ni rafiki yake, Rose.

Sarah aliondoka eneo lile akiwa amepooza mwili kama mtu aliyemwagiwa maji

katikati ya upepo wa kipupwe. Aliondoka akiendelea kujiwazia na kuweka mikakati sawia ya kuusaka mwanzo mpya wenye amani zaidi.

Kwa waliofanikiwa kumuona Sarah, hawakuacha kumtamani. Vijana wengi wa kijijini hapo, walitamani sana kuonja penzi lake wakiamini ingekuwa ni tunu kupata penzi la bibie yule aliyerejea katika siku za karibuni kutoka mjini. Wengi, walikuwa wameanza kumsahau. Wengine walimkumbuka lakini walishangazwa na uzuri wake kuongezeka mara dufu ya vile alivyokuwa pindi alipoondoka kwa mara ya mwisho.

Sarah, aliyekuwa mzoefu wa kubadili na kuchanganya wanaume atakavyo, bado hakutaka kuwa mchoyo. Wachache waliomtaka aliwatoza pesa kuwapatia penzi lake. Wafanyabiashara wa kwenye magulio, wakulima wa mashamba ya mpunga na mahindi, pamoja na matajiri waliomiliki mifugo, ndiyo waliokuwa kipaumbele chake. Alivuna pesa, pasina kujali nini kingefuata mbele. Ni psea hizo ndizo ziliendesha maisha yake katika wakati ule aliorejea kutoka mjini. Uzuri wake ulihitaji matunzo makubwa, hivyo pia mara nyingine aliagiza vipodozi na mapambo kutoka mjini kwa ajili ya kujiboresha.

*                    *                    *

Mwili wa Sarah ulitota kwa jasho lililomtoka kwa wingi wake. Alionekana kujichokea kidogo, huku akiwa amefurahia huduma safi aliyopatiwa na kijana mmoja ambaye kwa kipindi kirefu aliwahi kumtaka Sarah kimapenzi, huyu aliitwa Isaya.

Naye Isaya alikuwa amejilaza chali akihemea juu juu, mwili wake ukirejesha nguvu taratibu baada ya kuzipoteza kwa kushughulika na mwili wa Sarah. Mtibuano ulikuwa mkali kiasi kwamba chumba kile alichoishi Isaya hakikuweza kutazamika. Nguo zilitupwa hovyo, vitu vilipoteza mpangilio stahiki. Lakini, hilo halikuwa na tija kwake Isaya, yeye alijipongeza kwa kufanikiwa kutimiza ndoto yake ya kula fungate na Sarah.

Isaya aligeuka kidogo kumtazama Sarah, kumbe naye Sarah alikuwa akimtazama Isaya, basi macho yao yakagongana kiasi cha kuwafanya watoe vicheko laini. Mara, Isaya akainua mkono kupapasa kalio la Sarah, akalamba midomo kwa uchu, akipagawa kwa kushika 'dude' kubwa kama lile.

"We' Isaya, uchokozi huo ujue..!!". Alisema Sarah kwa sauti nyenyekevu haswa. Akasikia raha kwa jinsi kiganja cha Isaya kilivyojitembeza juu ya ngozi ya kalio lake. Akashituka kidogo, kwa maana kuna muda alichombezwa kidogo na vidole vya Isaya.

"Sarah, huu mzigo wako nilikuwa nautamani kwa kitambo kirefu sana..! Siamini kama leo umenipa 'nijipakulie' mwenyewe..!!".

"Aiiihh..!! Eti 'mzigo'...!!". Alisema Sarah akificha sura. Alijilaza kifudifudi kuruhusu kiuno chake kibinuke zaidi na nyama nyingi za nyuma yake kuinuka juu kama kichuguu.

"Leo hutoki, Sarah. Sikuachi uondoke hadi ikifika jioni..!".

"Wewe tu, mpenzi..! Nishike unirarue hadi nirukwe na akili...!". Alisema Sarah, bila kujua kama alikuwa akizidi kumchanganya Isaya. Kidume huyo akacheka hata lile jino lake lililomegeka kipande likaonekana. Mara akaanza kumchekecha Sarah kwa matembezi ya huku na kule kwenye mwili wake. Sarah alijikunja huku akisema maneno yasiyoeleweka. Mara, Isaya akashika bakora yake na kutaka kuzamisha katikati ya mzinga wa asali, lakini Sarah akaleta ugumu kidogo..

"Kabla hatujaendelea, naomba uniahidi kitu..!!".

"Kitu gani tena, mama..!?"..

"Naomba uniahidi kuwa utanikutanisha na Allen..!".

"Ah..! Kwahiyo unataka nikukutanishe na bwana wako umpe utamu, siyo..!?". Aliuliza Isaya kwa gadhabu.

"Siyo hivyo, Isaya. Mbona nina mwaka mzima tangu kuachana kwetu na Allen..! Mimi nina jambo langu na Allen...!".

"Jambo gani hilo..!?".

"Allen ana deni langu, tena la pesa kubwa. Nilimpatia wakati tulipokuwa kwenye mahusiano, sasa tumeachana na bado ananizungusha..!".

"Sawa...!! Kama ni hivyo, nitakusaidia jinsi ya kuonana naye..!!". Alisema Isaya, huku akiharakisha kupachika mkuki. Sarah akaitika kidogo akiupokea mshindo wa Isaya.

"Isss....!! Isa....ooohh.....jamaniiii..!! weeewweee...!! Ah...! Taamuuuuu..!Yeesss...ah..!". Alisikika Sarah akiendelea kufurahia pilika na fujo za Isaya. Sarah akajibinua kidogo kiuno chake kiweze kuinuka, akilikamata shuka na kulifinya kwa nguvu. Isaya akaachia kofi la kimahaba lililochapa minofu ya Sarah, minofu ikacheza kuitika mikito ya kijana huyo mwenye nguvu.

*                    *                    *

Halaiki ya wanakijiji ilikuwa imekusanyika kukizingira Kiwanja cha shule ya msingi Pambazuko, wakifurahia burudani ya mchezo wa mpira wa miguu iliyokuwa ikiendelea. Waliokosa nafasi za kusimama walipanda juu ya miti ili wapate uoni angavu. Wazee kwa vijana, na hasa wanaume wa kijiji kile walikuwa na jambo kubwa lililowakutanisha siku hiyo.

Miongoni mwao, alikuwepo Allen. Alituama sehemu akifurahia kutazama mchezo ule uliokuwa na mvuto wa aina yake. Ulikuwa ni utaratibu wake kuhudhuria katika uwanja ule kupata burudani. Si hivyo tu, pia aliwahi kucheza katika timu ya kijiji, kabla ya kutingwa

na mabadiliko ya maisha yaliyomsafirisha kwenda mbali kutafuta riziki. Akiwa katikati ya utulivu wake, mara akashikwa bega, na akajuzwa kuwa alikuwepo mtu aliyesimama nyuma akihitaji kumuona.

Alijitenga na ule umati, ndipo alipomuona Isaya akimsubiri. Isaya, aliyewahi kushiriki pamoja na Allen katika michezo mbalimbali kama wachezaji wa kutegemewa na kijiji, alionekana kutabasamu kidogo akimsubiri Allen amfikie karibu ili asalimiane naye kwa mapana zaidi. Na kweli, Allen alipofika alisalimiana na Isaya huku wakionesha kuchangamkiana kwa kiasi kikubwa.

Isaya, akamshika mkono rafiki yake, kisha kusogea naye pembeni kisha kwa ufupi tu akamueleza kuwa alikuwa na mazungumzo marefu ya kumuhusu Allen pia. Allen akakubaliana naye, wakaondoka na kuelekea mbali kabisa na ule mkusanyiko wa watu. Wakasimama wakiwa njiani kisha wakatulia kuyaanza mazungumzo yao.

"Kaka, huyo mtu unayesema anataka kuniona yuko wapi..!?".

"Subiri kaka, punde tu tutakuwa naye hapa..!!".

Wakati Allen na Isaya wakiendelea kusubiri ujio wa mtu huyo aliyetajwa, wakaendelea na mazungumzo ya haoa na pale huku wakichagiza kwa matani ya hapa na pale, kutokana na urafiki waliowahi kuwa nao kwa miaka mingi iliyopita.

Lakini, punde tu, alitokea Sarah, tena alitokea kwa mshitukizo kiasi cha Allen kutotarajia kama angemuona bibie huyo. Allen akabadilika ghafla, sura yake ikapoteza uchangamfu wa awali, na matani yote yakamuishia kinywani. Alichefuliwa nafsi yake kwa kuletewa Sarah mbele ya macho yake.

"Isaya, kwahiyo umenitoa kule uwanjani hadi hapa, ili uje kunikwaza au sio..!? Umeona halitoshi kukatisha burudani yangu, na sasa unanitia majaribu kama haya..!? Eenh..!?". Aling'aka Allen kwa sauti, kiasi cha kumfanya hata Isaya ajitulize kidogo kupanga sera za kusema.

"Hapana, kaka. Siyo kama unavyodhani...! Sikupanga kukukwaza wala kukatisha burudani yako..! Kwanza naomba utulize jazba, ndugu yangu..!".

"Ndiyo, Allen..!! Naomba utulie unisikilize mwenzako. Ni mimi ndiye niliyemuomba Isaya anikutanishe na wewe. Kwahiyo, kama ni lawama naomba unipe mimi..!!". Sarah aliingilia kati, akiyalengesha macho yake kwenye uso wa Allen.

"Tena we' mpuuzi ndiyo ukae kimya kabisa..!! Usiseme chochote, maana sitaki kusema chochote na wewe..!!". Allen alimkaripia Sarah.

"Msikilize bhana..!! Mbona unakosa ustaarabu, ndugu yangu..!?". Aliuliza Isaya huku akichukizwa na makasiriko ya Allen.

"Halafu, naomba usijiingize kwenye mambo yasiyokuhusu. Hujui nini kinacheondelea, basi usipige kelele kama kengele mbovu..!! Tuheshimiane, Isaya...!! Tuheshimiane..!!". Kikichomkuta Sarah, ndicho kilihamia kwa Isaya. Allen alipaza sauti 'kukoroma' huku mishipa ya shingo ikichachamaa. Si Isaya wala Sarah aliyonekana kuweza kumtuliza Allen. Hata alipotaka kuondoka, Isaya alitulia kimya, lakini Sarah akaonesha uthubutu kwa kumkamata mkono.

Ni heri asingejaribu, ni heri asingemshika Allen...kwa maana alijiponza kwa kufanya hivyo. Allen aliachia kofi kali lililompata vema Sarah. Ukelele wa maumivu ukamtoka Sarah akijikuta anaacha mkono na kujiziba uso wake. Ikamlazimu Isaya aokoe jahazi kwa kuingilia kati. Allen akaondoka zake akitema misemo ya kikafiri, akimuacha Sarah akiwa analia angali amejilaza katika kifua cha Isaya.